



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



IMETHIBITISHWA ISO 9001

TAARIFA KWA UMMA

MWALIKO WA MKUTANO WA KUPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU MCHAKATO WA MAPITIO YA NAULI ZA USAFIRI WA UMMA KWA NJIA YA BARABARA- UKUMBI WA KARIMJEE, DAR ES SALAAM

Dar es Salaam, 04 Aprili 2026

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kwa kuzingatia Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 huandaa na kufanya mapitio ya tozo mbalimbali za huduma za usafiri ardhini zinazodhibitiwa ikiwemo nauli za usafiri wa umma kwa njia ya Barabara. Uandaaji wa tozo hizo huzingatia mazingira mbalimbali ikiwemo maslahi ya Watumia Huduma na Watoa Huduma. Katika kipindi cha hivi karibuni, kumetokea ongezeko la bei ya mafuta (petroli na dizeli) kwa takribani Shilingi za Kitanzania 950 kwa lita moja. Endapo sababu za bei ya mafuta kupanda zitaendelea kuwepo, bei ya mafuta nayo itaendelea kuongezeka, na hivyo itaathiri gharama za uendeshaji kwa Watoa Huduma na utoaji wa huduma za usafiri kwa ujumla. Kutokana na hali hii, tarehe 1 Aprili 2026, LATRA ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari ya kuitisha mkutano wa wadau utakaofanyika Jumatano, tarehe 08 Aprili 2026, Dar es Salaam.

Kanuni za Tozo za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2020 (GN Na. 82 ya tarehe 7/2/2020) zinaelekeza utaratibu wa **Mtoa Huduma kuwasilisha mapendekezo ya mapitio ya nauli** au **Mamlaka kuanzisha mchakato pale inapobidi**, ili kuhakikisha kuwa nauli zinaakisi gharama halisi za uendeshaji na kulinda uendelevu wa huduma za usafiri wa umma. Kutokana na hali hii, LATRA imeandaa mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu hatua za kuchukuliwa endapo gharama za mafuta zitaendelea kuongezeka. Maoni hayo yataisaidia Mamlaka katika kufanya mapitio ya nauli za huduma za usafiri wa umma kwa njia ya Barabara. Mkutano utafanyika siku ya **Jumatano, tarehe 08 Aprili 2026, katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, kuanzia saa 3:30 asubuhi**. Aidha, wadau watakaoshindwa kuhudhuria, wataweza kushiriki kwa njia ya mtandao (online) kupitia LATRA Online TV.

Hivyo, **LATRA inawaalika Wadau wote wa usafiri ardhini kuhudhuria mkutano huu muhimu**. Watakaotaka kufanya wasilisho au kutuma maoni, watume kwa njia ya barua pepe dg@latra.go.tz au info@latra.go.tz

Imetolewa na:

CPA, Dkt. Habibu J. S. Suluo

MKURUGENZI MKUU